# VIWANGO VYA UCHANGIAJI WA VIFURUSHI VYA BIMA YA AFYA

| NA. | UKUBWA WA FAMILIA | MCHANGIAJI KUANZIA MIAKA 18- 35 | | | MCHANGIAJI KUANZIA MIAKA 36 - 59 | | | MCHANGIAJI KUANZIA MIAKA 60+ | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | NAJALI AFYA | WEKEZA AFYA | TIMIZA AFYA | NAJALI AFYA | WEKEZA AFYA | TIMIZA AFYA | NAJALI AFYA | WEKEZA AFYA | TIMIZA AFYA |
| 1 | Mtu mmoja | 192,000 | 384,000 | 516,000 | 240,000 | 444,000 | 612,000 | 360,000 | 660,000 | 984,000 |
| 2 | Wanandoa | 384,000 | 732,000 | 996,000 | 456,000 | 864,000 | 1,188,000 | 684,000 | 1,284,000 | 1,908,000 |
| 3 | Wanandoa + Mtoto 1 | 504,000 | 924,000 | 1,272,000 | 576,000 | 1,068,000 | 1,464,000 | | | |
| 4 | Wanandoa + Watoto 2 | 612,000 | 1,116,000 | 1,536,000 | 696,000 | 1,248,000 | 1,728,000 | | | |
| 5 | Wanandoa + Watoto 3 | 720,000 | 1,284,000 | 1,788,000 | 804,000 | 1,416,000 | 1,980,000 | | | |
| 6 | Wanandoa + Watoto 4 | 816,000 | 1,452,000 | 2,028,000 | 900,000 | 1,584,000 | 2,220,000 | | | |
| 7 | Mtu mmoja+ Mtoto 1 | 312,000 | 576,000 | 792,000 | 360,000 | 648,000 | 888,000 | | | |
| 8 | Mtu mmoja+ Watoto 2 | 432,000 | 756,000 | 1,056,000 | 468,000 | 828,000 | 1,152,000 | | | |
| 9 | Mtu mmoja+ Watoto 3 | 540,000 | 924,000 | 1,308,000 | 576,000 | 996,000 | 1,404,000 | | | |
| 10 | Mtu mmoja+ Watoto 4 | 636,000 | 1,092,000 | 1,548,000 | 672,000 | 1,164,000 | 1,644,000 | | | |

## JINSI YA KUJISAJILI

- Mwanachama anatakiwa kujaza fomu ya kujiunga ambayo inapatikana katika ofisi za Mfuko nchi nzima au kupitia tovuti ya Mfuko www.nhif.or.tz
- Mwanachama anatakiwa kuwa na namba ya kitambulisho cha Taifa
- Mwanachama atapaswa kuwa na picha moja ya rangi ya ukubwa wa passport size,
- Mwanachama anayemwandikisha mwenza atahitajika kuambatanisha picha moja ya mwenza ya rangi, nakala ya cheti cha ndoa pamoja na namba ya kitambulisho cha Taifa.
- Mwanachama anayemwandikisha mtoto kama mtegemezi atahitajika kuambatanisha picha ya mtoto na nakala ya cheti cha kuzaliwa cha mtoto. Tangazo la kuzaliwa linaweza kuwasilishwa kama mbadala wa cheti cha kuzaliwa endapo mtoto ana umri wa chini ya miezi 6.
- Mwanachama atapewa namba ya malipo (control number) ambayo ataitumia kufanya malipo kupitia benki au mitandao ya simu.
- Mwanachama atafanya malipo yote kwa mkupuo au kwa awamu kupitia utaratibu maalum wa benki
- Mwanachama atapatiwa kitambulisho cha matibabu na kuanza kupata huduma zilizoainishwa katika kifurushi alichokichagua kwa kuzingatia vigezo na masharti yaliyowekwa.
- Mwanachama anaweza kujisajili kupitia mtandao, ili kujisajili tembelea tovuti ya Mfuko www.nhif.or.tz ukiwa na namba ya kitambulisho cha Taifa ili kukamilisha usajili wako.

**Huduma kwa Wateja Piga Simu bila Malipo**
**0800 110063.**

NATIONAL HEALTH INSURANCE FUND NHIF ISO 9001:2015 CERTIFIED

**MFUKO WA TAIFA WA BIMA YA AFYA**




# VIFURUSHI
## vya Bima ya Afya

*Uhakika wa Matibabu kwa Wote*

TOLEO LA MEI 2021

www.nhif.or.tz | Piga **0800 110063** bure | nhiftz | NHIF ONLINE TV

## VIJUE VIFURUSHI VYA BIMA YA AFYA

Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) umepanua wigo wa mafao yake kwa kuanzisha vifurushi vya bima ya afya ili kuwapa fursa wananchi wengi zaidi kujiunga na kunufaika na huduma za bima ya afya nchini. Vifurushi hivi vinatoa fursa kwa mtu mmoja mmoja au familia kujiunga kwa kuzingatia vigezo na masharti yaliyowekwa na

Mpango huu umewekwa kwa utaratibu wa vifurushi vya NAJALI AFYA, WEKEZA AFYA na TIMIZA AFYA ambao unamwezesha mwananchi kuwa na uhakika wa kupata huduma za matibabu bila kikwazo cha fedha hivyo kumudu gharama za matibabu ambazo zimekuwa zikiongezeka siku

## MADHUMUNI YA VIFURUSHI

- Kutoa fursa kwa wananchi walio katika sekta isiyo rasmi wenye umri wa kuanzia miaka 18 na kuendelea pamoja na wategemezi wanaokubalika kuweza kunufaika na huduma za matibabu.
- Kutoa fursa kwa wananchi wengi zaidi kupata huduma za matibabu kwa gharama nafuu.

## MWANACHAMA WA VIFURUSHI ATANUFAIKA NA NINI?

Mwanachama wa Mfuko kupitia vifurushi atapata huduma katika vituo vyote vya umma, binafsi na vya mashirika ya dini vilivyosajiliwa na Mfuko nchi nzima kuanzia ngazi ya zahanati hadi hospitali ya rufaa ya taifa. Hata hivyo, mwanachama atahitaji rufaa kwenda ngazi ya hospitali za rufaa za kanda na hospitali ya rufaa ya Taifa. Mwanachama wa Vifurushi atanufaika na mafao yafuatayo:-

- Ada ya kujiandikisha na kumuona daktari,
- Huduma za vipimo,
- Huduma za Dawa zinazoruhusiwa kwenye ngazi husika,
- Huduma ya kulazwa,
- Huduma za upasuaji mdogo na upasuaji mkubwa,
- Huduma za uzazi kwa kuzingatia vigezo na masharti yaliyowekwa.

## MAFAO KWA WANUFAIKA WA NHIF KUPITIA VIFURUSHI VYA BIMA YA AFYA

| NA | MAFAO | Huduma Zinazopatikana Katika Vifurushi Vya Bima ya Afya | | |
|---|---|---|---|---|
| | | NAJALI AFYA | WEKEZA AFYA | TIMIZA AFYA |
| 1. | Ada ya kujiandikisha na kumwona daktari | Inalipiwa katika ngazi zote za vituo. | Inalipiwa katika ngazi zote za vituo. | Inalipiwa katika ngazi zote za vituo |
| 2. | Huduma za kulazwa | Inapatikana kwa jumla ya siku zisizozidi 30 kwa mwaka kwa kila mnufaika mmoja. | Inapatikana kwa jumla ya siku zisizozidi 45 kwa mwaka kwa kila mnufaika mmoja. | Inapatikana kwa jumla ya siku zisizozidi 60 kwa mwaka kwa kila mnufaika mmoja. |
| 3. | Huduma za dawa | Dawa zote zilizoainishwa katika Kitita cha Mafao cha NHIF Daraja A, B, C, D na S | Dawa zote zilizoainishwa katika Kitita cha Mafao cha NHIF Daraja A, B, C, D na S | Dawa zote zilizoainishwa katika Kitita cha Mafao cha NHIF Daraja A, B, C, D na S |
| 4. | **VIPIMO VYA MAABARA NA UCHUNGUZI** | | | |
| | Aina za Vipimo | 162 | 197 | 223 |
| | X-RAY | Inapatikana | Inapatikana | Inapatikana |
| | ECHO & EEG | Inapatikana | Inapatikana | Inapatikana |
| | Ultrasound | Inapatikana | Inapatikana | Inapatikana |
| 5. | **HUDUMA ZA KINYWA NA MENO** | | | |
| | Kung'oa na kuziba meno | Inapatikana | Inapatikana | Inapatikana |
| 6. | **HUDUMA ZA UZAZI** | | | |
| | Kujifungua kawaida | Inapatikana baada ya kuchangia mfululizo katika kipindi cha miaka miwili. | Inapatikana kuanzia mwaka wa pili wa kuchangia mfululizo. | Inapatikana kuanzia mwaka wa pili wa kuchangia mfululizo. |
| | Kujifungua kwa upasuaji | Inapatikana baada ya kuchangia mfululizo katika kipindi cha miaka miwili. | Inapatikana kuanzia mwaka wa pili wa kuchangia mfululizo. | Inapatikana kuanzia mwaka wa pili wa kuchangia mfululizo. |
| 7. | **HUDUMA ZA MATIBABU YA KIBINGWA** | | | |
| | Huduma za kibingwa | Zinapatikana mpaka ngazi ya Hospitali za Mkoa na kwa rufaa hadi Hospitali za Rufaa za Kanda na Taifa. | Zinapatikana mpaka ngazi ya Hospitali za Mkoa na kwa rufaa hadi Hospitali za Rufaa za Kanda na Taifa. | Zinapatikana mpaka ngazi ya Hospitali za Mkoa na kwa rufaa hadi Hospitali za Rufaa za Kanda na Taifa. |
| 8. | **HUDUMA ZA UPASUAJI** | | | |
| | Aina za upasuaji mdogo | 27 | 30 | 50 |
| | Aina za upasuaji mkubwa | 14 | 36 | 80 |

Vigezo na Masharti Kuzingatiwa